

Kujifunza kutoka nyumbani ikiwa shule inafungwa

Kusaidia kujifunza kwa mtoto wako nyumbani

Majukumu ya mzazi wakati wa kujifunza kwa mbali

Toa msaada kwa watoto wako kwa njia za:

- kuanzisha utaratibu na matarajio
- Kuweka nafasi maalum kwa mtoto wako kufanya shughuli zake
- kuangalia mawasiliano kutoka walimu wa mtoto wako
- kuanza na kumaliza kila siku kwa kuuliza juu ya masomo ya mtoto wako
- kufanya jukumu kubwa katika kuwasaidia watoto wako na kukifunza kwao
- kuhimiza shughuli za kimwili na/au mazoezi
- kukumbuka kuwa mtoto wako anaweza kusisitizwa au kuwa na wasiwasi wakati huu
- kufuatilia ni muda gani mtoto wako anaotumia mtandaoni
- Kuendeleza watoto wako kuwasiliana na wengine, lakini kuweka sheria kuhusu mwingiliano wao wa mitandao ya kijamii.

Majukumu ya wanafunzi wakati wa kujifunza kwa umbali

Majukumu haya yanapaswa kubadilishwa kulingana na umri wa mtoto wako:

- kuanzisha na/ au kufuata utaratibu wa kila siku kwa kujifunza
- kufanya shughuli katika nafasi salama ya raha na utulivu katika nyumbani kwao ambayo imewekwa maalum kwa ajili yao
- kuangalia programu na mawasiliano za dijiti mara kwa mara ili kuangalia kwa matangazo na majibu kutoka walimu
- kufanya shughuli kwa uaminifu na kufanya shughuli zao vizuri
- kufanya bidii kufikia malengo ya wakati, ahadi, na tarehe za wakati wake
- kuwasiliana na walimu wao ikiwa hawawezi kufikia tarehe ya mwisho au wakihitaji msaada zaidi
- kushirikiana na kuwasaidia wanafunzi wenzao kwenye masomo yao
- kufuata [Student use of digital devices and online services policy \(Sera ya matumizi ya wanafunzi ya vifaa vya dijiti na huduma za mtandaoni\)](#) ya idara
- kuwasiliana na wafanyikazi wa shule wakati mahitaji tofauti yanapotokea.

Kupanga siku ya mtoto wako

Shule yako inapaswa kumpa mtoto wako na ratiba ya masomo yake. Hii ni pamoja na mapumziko ya kila mara kwa shughuli, kula na kunywa. Katika mapumziko ya shughuli ni muhimu wanafunzi wainuke na kuzunguka.

Ikiwa unaishi katika nyumba ya kibinafsi, basi ni salama kwa mtoto wako kwenda nje kwenye bustani, ubaraza wa ghorofani au uwanja.

Ustawi

Kufungwa nyumbani kwa muda mrefu kunaweza kusababisha kusesitizwa na migogoro. Vidokezo vya kutunza watoto wako wakati wa kutengwa ni pamoja na:

- kuzungumza na familia nzima yako kuhusu maambukizi - kuelewa hali hiyo kutapunguza wasiwasi
- kuwasaidia watoto wako kufikiria juu ya jinsi walivyovumilia hali ngumu zamani na kuwapa moyo kuwa watavamila hali hiyo pia
- kuwakumbusha kuwa kutengwa hakutaendelea kwa muda mrefu
- kufanya mazoezi kila mara - mazoezi ni tiba iliyothibitishwa kwa msisitizo na majonzi.
- kuwatia moyo watoto wako kuwasiliana na wanafamilia na marafiki kwa njia ya simu, barua pepe au mitandao ya kijamii (inapowezekana).

Kuwasiliana

Kuwasiliana na mtoto wako

Tunakutia moyo uanze na kumaliza kila siku na maswali rahisi machache kuhusu masomo ya mtoto wako ili kuwasaidia kupanga siku yake. Sio wanafunzi wote wanaofaulu katika mazingira ya kujifunza kwa mbali; wengine wanapambana na uhuru mwingi au ukosefu wa mipango na maswali yako yatasaidia kuwaendelea na shughuli zao.

Kuwasiliana na shule

Hakikisha unajua jinsi ya shule na walimu wa mtoto wako watakavyowasiliana nawe na angalia njia hiyo mara kwa mara.

Hakikisha unajua jinsi ya kuwasiliana na walimu kwa msaada wa masomo na kuwasiliana na nani kupata msaada wa ufundi ikiwa shule yako itachagua kutumia vifaa vya dijiti kama sehemu ya mpango wao wa kujifunza kwa mbali.

Hali hii itakuwa mpya kwa shule na familia nyingi. Shule zitajaribu kushiriki katika mzunguko wa uboreshaji unaoendelea kulingana na majibu kwa hiyo waweze kuuliza wewe na mtoto wako kwa maoni juu ya jinsi mfumo unavyofanya kazi.

Shule nyingi tayari zinatumia aina fulani ya programu ili kuwasiliana na wazazi na wanafunzi. Programu hayo yaliyopo yanapaswa kuendelea kutumikwa wakati inapowezekana.

Kuwasiliana na walimu

Walimu wanaweza kupanga wakati fulani ambapo wanafunzi wanaweza kuzungumza nao mtandaoni, kutoa masomo ya video au kama chaguzi za dijiti haziwezekani wanaweza kupanga wakati fulani wa kupiga simu kwa mtoto wako.

Ni muhimu kwako na kwa mtoto wako kukumbuka kuwa walimu watakuwa wanawasiliana na familia zingine nyingi, kwa hivyo mawasiliano yako yanapaswa kuwa muhimu na mafupi. Unaweza pia kuhitaji kumkumbusha mtoto wako kuwa mwenye subira wakati wa kungojea msaada au majibu.

Kutumia teknolojia

Kununua programu au vifaa vipya

Inashauriwa sana kuwa wazazi wasinunue programu kutoka kwa watoa huduma wa tatu kwa kujibu hali hii isipokuwa unashauriwa haswa na shule.

Shule yako na idara tayari zina programu na vifaa mbalimbali zinazopatikana na hizi zimechaguliwa haswa kumpa mtoto wako msaada wanaohitaji.

- Google Apps for Education – Online Google apps. Kwa ufikiaji wa wanafunzi nenda kwa: Students portal > Learning > G Suite.
- Office 365 – online Office apps.
- Microsoft Office 365 Desktop Apps – inaweza kusanikishwa hadi kompyuta tano na vifaa kumi vya mkononi. Chagua kiunga cha 'Install Office'.
- Wanafunzi wanaweza pia kupata programu bure ya ziada ya Adobe kwa vifaa vyao kutoka tovuti ya wanafunzi kwa programu Bring your own device (BYOD) ('Leta kifaa chako').

Kupata vifaa vya dijiti na mtandao

Sera ya idara kuhusu teknolojia, vifaa na mtandao inapatikana kwenye kiunga kifuatacho.

[Student use of digital devices and online services policy \(Sera ya matumizi ya wanafunzi ya vifaa vya dijiti na huduma za mtandaoni\)](#)

Ikiwa mtoto wako atakuwa anatumia rasilimali za dijiti kama sehemu ya masomo yao na hawana hakika jinsi ya kufanya hivyo wanapaswa kuwasiliana na mwalimu wao wa darasa ili kupata msaada.

Kusimamia wakati wa skrini

Kuna mipaka juu ya kiasi cha wakati ambao mtu yeyote atumie mtandaoni, lakini viwango na sheria za wakati wa skrini zinatofautiana na umri.

Mikutano ya video na mwingiliano wa kijamii kwa kutumia video hakuhesabu katika wakati wa skrini.

Nyakati zifuatazo za skrini zilizopendekezwa (ukiondoa mikutano ya video) zinategemeza mapendekezo kutoka Chuo cha Uganga wa Watoto cha Amerika:

- Umri wa miaka 2-5: muda wa saali 1 jumla, kugawaniwa katika vikao visivyozidi dakika 30.
- Umri wa miaka 6 na juu: hakuna mipaka maalum ya wakati wa skrini, lakini wakati wa skrini unapaswa kutoathiri shughuli za kimwili na mwingiliano wa uso-kwa-uso kwa nyumbani na shuleni (inapowezekana). Ni muhimu sana kuwa mwaminifu na mipaka yako ya wakati wa skrini.

Hakikisha kuwa shughuli zisizo za shule haendi kwa muda mrefu.

Kusimamia tabia

Hata ingawa mtoto wako yupo nyumbani bado wanahitaji kutii sera ya usimamizi wa tabia ya shule yake.

Kushirikiana, shughuli ya kikundi na majibu ya rika wakati wa kujifunza kwa mbali itahitaji wanafunzi kuwasiliana mtandaoni na kushiriki pamoja katika nafasi za dijiti. Matarajio ya mtoto wako na tabia inayohitajika itakuwa sawa na somo la uso-kwa-uso.

Huduma ya Ukalimani wa Simu

Ikiwa unahitaji habari zaidi tafadhali piga simu kwa mwalimu mkuu wa shule yako. Ikiwa unahitaji mkalimani kukusaidia na swali lako tafadhali piga simu Huduma ya Ukalimani wa Simu kwenye 131 450 na uombe mkalimani wa lugha yako. Huduma hii itakuwa bure kwako.